Siku ya Mazingira Duniani Mwaka wa 2023

# Komesha Uchafuzi wa Plastiki

## MWONGOZO WA VITENDO

KOMESHA UCHAFUZI WA PLASTIKI

SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI

UN environment programme

Republic of Côte d'Ivoire

Supported by

Ministry of Infrastructure and Water Management of the Netherlands

# Content


**Tatizo hili ni kubwa kwa kiwango gani?** .......... **3**

Uchumi .......... 4

**Je, tunawezaje kutatua tatizo la uchafuzi wa plastiki?** .......... **5**

Watu binafsi .......... 5

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, mashirika ya kidini na vikundi vya kijamii .......... 6

Mashirika ya sayansi na elimu .......... 7

Serikali .......... 8

Majiji, miji na serikali za mitaa .......... 9

Fedha .......... 10

Biashara na viwanda .......... 11

**Je, uchafuzi wa plastiki unaathiri vipi bayoanuwai, tatizo la tabianchi, wanyamapori, na afya ya binadamu?** .......... **12**

Bayoanuwai .......... 12

Tatizo la tabianchi .......... 12

Afya ya binadamu .......... 12

**Je, takataka hizi zote za plastiki hutoka wapi?** .......... **13**

Upakiaji .......... 13

Utengenezaji wa Bidhaa .......... 13

**3**Majengo na ujenzi .......... 14

Kilimo .......... 14

Uvuvi .......... 14

Nishati, mafuta na gesi .......... 14

Nguo na mtindo .......... 14

Usafiri na utalii .......... 14

Uchukuzi .......... 14

**Hatua gani zimepigwa?** .......... **15**

**Ni nini kingine kinachohitajika kufanywa?** .......... **16**



*Ocean Image Bank*

# Tatizo hili ni kubwa kwa kiwango gani?

**Uchafuzi wa plastiki unaweza kuzuilika. Kuchukua hatua katika sekta zote za jamii kunaweza kusitisha na kuirejesha hali iliyokuwepo hapo awali. Mwongozo huu unatoa vidokezo vya jinsi sote tunaweza kuwa sehemu ya vuguvugu la kimataifa la #KomeshaUchafuziWaPlastiki.**

Tuna mazoea ya kutumia plastiki. Tunazalisha takriban tani milioni 430 za plastiki kwa mwaka, theluthi mbili kati yake ni bidhaa za muda mfupi ambazo hufanywa takataka baada ya muda mfupi. Uchafuzi wa plastiki unaweza kuwa na madhara mabaya kabisa kwa mifumo yetu ya ekolojia na wanyamapori, afya na ustawi wetu na uchumi wa kimataifa.

Walakini, ahadi za sasa zilizotolewa na serikali na viwanda zitapunguza tu kiwango cha kila mwaka cha plastiki zinazoingia baharini kwa asilimia 8 kufikia mwaka wa 2040. Gharama za kijamii na kiuchumi za uchafuzi wa plastiki hufikia hadi dola bilioni 600 za Marekani kwa mwaka.

Licha ya gharama hizi, tunaendelea kuzalisha plastiki zaidi na zaidi – matumizi ya plastiki yamejikita katika kila nyanja ya maisha ya kisasa. Tunazitumia katika magari yetu, nyumbani mwetu, kwenye vifaa vya matibabu, nguo na shampuu. Ingawa matangazo mengi ya uchafuzi wa plastiki katika vyombo vya habari yanaangazia taswira zinazovunja moyo za wanyamapori wakisakamwa na mifuko ya plastiki, ukweli ni kwamba uchafuzi wa plastiki una madhara mengi hata zaidi. Uchafuzi mwingi wa plastiki hauonekani kwa macho. Mikroplastiki – vipande vidogo vya plastiki vilivyo chini ya mm 5 kwa urefu – vinachafua udongo, maji na miili yetu.



Shutterstock

## Maelezo ya ziada: kwa nini plastiki inatumika sana?


Haishangazi kwamba plastiki inatumika sana: ni nafuu kuzalisha, hudumu, hunyumbulika kwa urahisi na ni rahisi kusafirisha. Plastiki imetengenezwa kutoka kwa mafuta ya visukuku, ilianza kuzalishwa kwa wingi wakati wa Vita vya Pili vya Dunia. Uchimbaji wa mafuta ya visukuku ulipotoa malighafi kwa uzalishaji wa plastiki, kila kitu kutoka kwa vifaa vya nyumbani hadi vifaa vya matibabu vilitengenezwa kwa kutumia plastiki. Uzalishaji wa plastiki umeongezeka zaidi katika kipindi cha miaka 50 iliyopita na unatarajiwa kuongezeka maradufu katika kipindi cha miaka 20 ijayo, na ikiwa hatua hazitachukuliwa uchafuzi wa plastiki utaongezeka mara tatu zaidi kufikia mwaka wa 2060. Kutokana na sababu hii, ni muhimu kuanza kutumia uchumi thabiti inaotumia bidhaa tena na tena, ulio na manufaa zaidi kiuchumi haraka iwezekanavyo.

Uzalishaji wa gesi ya ukaa (GHG) unaohusishwa na mzunguko mzima wa plastiki uliwakilisha asilimia 3.4 ya idadi jumla ya kimataifa katika mwaka wa 2019. Athari zake kwa bayoanuwai (ikiwa ni pamoja na kunusa, kumeza kemikali hatari, n.k.) na kwa afya ya binadamu (k.m. kutokana na utoaji wa kemikali hatari kwenye mzunguko mzima wa plastiki) zinazidi kueleweka na ni za kiwango kikubwa sana. Katika hali ya kawaida, plastiki inaweza kutoa asilimia 19 ya uzalishaji wa gesi ya ukaa duniani kufikia mwaka wa 2040.

## Uchumi

Biashara ya kimataifa ya plastiki imepanuka na kufikia zaidi ya dola trilioni 1 za Marekani kila mwaka. Lakini, gharama za kiuchumi za uchafuzi wa plastiki ni za juu sana pia. Kuenea kwa takataka za plastiki hudhuru mifumo ya ekolojia na afya ya binadamu kwa thamani ya dola kati ya bilioni 300 na bilioni 600 za Marekani kwa mwaka.

Kuanza kutumia uchumi unaotumia bidhaa tena na tena kufikia mwaka wa 2040 kunaweza kuokoa zaidi ya Dola trilioni 4.5 za Marekani. Kutapunguza pia gesi ya GHG kwa asilimia 25 na kubuni nafasi 700,000 zaidi za ajira, hasa katika nchi zinazokua kiuchumi na kuboresha maisha ya mamilioni ya wafanyakazi katika sekta isiyo rasmi, hasa katika nchi zinazokua kiuchumi. **Kwa ufupi, kuhama kutoka kwa mtindo wa sasa usio endelevu ni bora kwa sayari, tabianchi, afya na uchumi wetu.**




UNEP / Duncan Moore, Florian Fussstetter

## Maelezo ya ziada: Mbinu ya kushughulikia mzunguko mzima ni nini?

**Tatizo la uchafuzi wa plastiki unatokana hasa na ukweli kwamba plastiki kwa sasa inazalishwa, kutumiwa (wakati mwingi mara moja tu) na kisha kutupwa. Kukabiliana na uchafuzi wa plastiki kunahitaji mbinu ambayo inashughulikia hatua zote za mzunguko wa plastiki, kutoka kwa uzalishaji, matumizi hadi udhibiti wa takataka, kupunguza uchafuzi wa mazingira na takataka katika kila hatua. Mbinu ya kushughulikia mzunguko mzima pia husaidia kusawazisha mahitaji ya kiuchumi na wasiwasi juu ya athari za uchafuzi wa plastiki.**

# Je, tunawezaje kutatua tatizo la uchafuzi wa plastiki?

**Kwa vile uchafuzi wa plastiki ni tatizo la kimataifa, kulitatua kunahitaji mbinu ya kimataifa. Kila mmoja wa wadau wafuatao ana wajibu wa kutekeleza.**

## Watu binafsi

**Vitendo vya mtu binafsi huunga mkono mabadiliko ya kimfumo yanayohitajika ili kuwa na uchumi usiotegemea plastiki zaidi. Kila mmoja wetu anaweza kutumia sauti na mamuzi yetu kuleta mabadiliko. Hapa kuna baadhi ya mambo unayoweza kufanya.**

- Hakikisha kuwa sauti yako inasikika. Ukiona kampuni ikitumia plastiki isiyohitajika (kama vile plastiki inayotumiwa kufunika matunda mara moja kwenye duka la mboga), zikashifu kwenye mitandao ya kijamii au uwasiliane nao moja kwa moja. Tumia pesa zako kuleta mabadiliko. Ikiwa una hazina ya ustaafu, unaweza kuwa unawekeza bila kukusudia katika tasnia zisizo endelevu. Muombe msimamizi wako wa hazina kuhamisha fedha zako hadi mahali ambapo pana uwajibikaji.
- Wajulishe wanasiasa kwamba unajali kuhusu suala hili na kwamba wanapaswa kujali ikiwa wangependa kupata kura yako.
- Zungumza na wawakilishi wa eneo lako kuhusu suala hili. Waambie wasajili mji au jiji lako kwenye Mpango wa Kupunguza Uchafuzi wa Plastiki Katika Miji, ambao huhamasisha majiji na maeneo kuzuia utupaji wa plastiki kwenye mazingira asilia.
- Shiriki masuluhisho unayoyapata. Ukipata suluhisho la kibunifu au ukisikia kuhusu kampuni inayoanza inayokabiliana na uchafuzi wa plastiki, waambie marafiki zako na utangaze mpango huo kwenye mitandao ya kijamii.
- Jitolee kufanya kazi na vikundi vya kukusanya plastiki vya eneo lako.
- Toa mchango kwa mashirika ya misaada ambayo yanafanya kazi kutatua tatizo la uchafuzi wa plastiki.
- Badilisha tabia yako ili kuepuka plastiki inayotumika mara moja inapowezekana.
- Enda kwenye duka la mboga na mifuko yako mwenyewe; Epuka kununua bidhaa zilizopakiwa kupita kiasi.
- Nunua bidhaa zenye dhamana za muda mrefu ambazo zinaweza kurekebishwa na uhakikishe kuwa unatafuta mchakataji wa kutegemewa wakati bidhaa inapofikia mwisho wa matumizi yake.
- **Usikate tamaa! Hatua zinapigwa na harakati hizi zinazidi kupamba moto. Hatua za kila mtu katika kukabiliana na uchafuzi wa plastiki ni muhimu.**


Pexels

# Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, mashirika ya kidini na vikundi vya kijamii

**Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGO), mashirika ya kidini na vikundi vya kijamii huleta mabadiliko makubwa duniani. Hivi ndivyo wanavyoweza kusaidia kukabiliana na uchafuzi wa plastiki.**

- Kuwahimiza wawakilishi wa eneo lako kutunga sheria zinazopunguza matumizi ya plastiki (hasa matumizi ya mara moja) na kuimarisha miundombinu ya uchakataji katika eneo lako.
- Kuhimiza kampuni na mashirika mengine kuepuka plastiki inayotumiwa mara moja na/au kwa muda mfupi katika mahali pako pa kazi, nyumbani, na kwenye mikutano au hafla.
- Kushiriki mawazo na utafiti ambao unaweza kusaidia kupunguza plastiki zinazotumika mara moja katika jamii za eneo lako.
- Kushinikiza wauzaji na watengenezaji bidhaa kupunguza plastiki inayotumika mara moja.
- Kujiunga na [Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu Uchafuzi wa Plastiki na Takataka za Baharini,] na utumie jukwaa la kidijitali kuungana na wanaharakati wengine, kubadilishana maelezo na kuonyesha juhudi zilizofanywa na mafunzo tuliyopata.
- Kuweka maeneo ya umma ya kupata maji bila malipo ofisini mwenu, katika maeneo ya umma na hafla zote ili kuhimiza watu waepuke kutumia chupa za plastiki za maji zinazotumika mara moja.



Dreamstime

# Mashirika ya sayansi na elimu




**Jumuiya ya wanasayansi na wasomi wanaweza kutumia ushawishi na maarifa yao kukabiliana na uchafuzi wa plastiki. Haya ni baadhi ya mambo wanayoweza kufanya.**

- Kushiriki sayansi na utafiti wa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP) kuhusu uchafuzi wa plastiki na wanafunzi na wafanyakazi wenzako.
- Kutoa jukwaa kwa wale wanaokabiliana na tatizo hili; waalike kuzungumza katika chuo kikuu chako au kushiriki matokeo ya utafiti wao na wafanyakazi wako.
- Kushirikiana na sekta ya plastiki kubuni masuluhisho mapya endelevu kwa tatizo la uchafuzi wa plastiki, kama vile polima endelevu zaidi.
- Kupiga marufuku plastiki zinazotumika mara moja kutoka shuleni au kwenye maduka madogo ya chuo kikuu na mabewa.
- Kutengeneza vikundi vya kufanya kazi pamoja katika utafiti na tasnia katika idara zote za chuo kikuu ili kubuni suluhu kutoka kwa mitazamo tofauti ya utafiti.
- Kuweka maeneo ya umma ya kupata maji bila malipo chuoni ili kuhimiza watu waepuke kutumia chupa za plastiki za maji zinazotumika mara moja.
- Kuhakikisha kuwa uwekezaji na fedha za malipo ya ustaafu unawiana na uwekezaji unaowajibikia mazingira na jamii.
- Kujiunga na Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu Uchafuzi wa Plastiki na Takataka za Baharini, na utumie jukwaa la kidijitali kuungana na wanaharakati wengine, kubadilishana maelezo na kuonyesha juhudi zilizofanywa na mafunzo yaliyopatikana.

# Serikali

**Utungaji wa sheria ni muhimu katika kukabiliana na tatizo la plastiki. Ingawa harakati za kutafuta masuluhisho lazima zihusishe kila sekta, serikali zinahitaji kuwa mstari wa mbele katika kuleta mabadiliko. Hizi ni baadhi ya njia ambazo serikali zinaweza kutumia kuchochea mabadiliko katika kiwango cha kimataifa, kikanda na ndani ya nchi.**

- Kushiriki katika mchakato wa Kamati ya Majadiliano ya Serikali Tofauti (INC) ili kuunda chombo cha makubaliano ya kisheria ambacho kinashughulikia uchafuzi wa plastiki, ikiwa ni pamoja na katika mazingira ya baharini.
- Kujitolea kuchukua hatua katika mzunguko mzima wa plastiki kupitia mipango kama vile Ahadi Mpya ya Uchumi wa Plastiki Ulimwenguni, ambapo serikali kutoka mabara yote tayari zinatekeleza hatua za kupunguza uzalishaji wa plastiki isiyohitajika na kujumuisha utumiaji wa plastiki tena na tena.
- Kuweka sheria za kuunga mkono mabadiliko hadi uchumi mpya wa plastiki: kuondoa plastiki ambazo hatuhitaji; kuvumbua ili kuhakikisha plastiki tunazohitaji zinaweza kutumika tena, kuchakatwa au zinaweza kuoza; na kusambaza plastiki zote tunazotumia ili kuziweka ndani ya uchumi na nje ya mazingira.
- Kuagiza utekelezaji wa mipango ya uwajibikaji pana wa mzalishaji wa bidhaa (EPR) ili kuhakikisha kuwa wazalishaji bidhaa wana vivutio sahihi vya kutengeneza bidhaa vinavyozuia bidhaa na mifuko ya plastiki inazotumika mara moja, na kwamba miundombinu ya kukusanya na kuchakata inapokea ufadhili unaohitajika (UNEP 2023). Kando na mifano mingi iliyofaulu ya mipango ya EPR barani Ulaya, nchi kama Chile, Nigeria, Afrika Kusini na Kenya zimebuni sheria za EPR.
- Kuwekeza katika miundombinu sahihi ya kuchakata na kushughulikia takataka.
- Ondoa ruzuku kutoka kwa mafuta ya visukuku. Kizuizi kikuu cha kufikia utumiaji wa tena na tena ni gharama ya chini kabisa ya moja kwa moja ya plastiki inayotokana na mafuta ya visukuku kutokana na ruzuku nyingi na uwekezaji mkubwa katika uzalishaji wa kemikali zinazotokana na mafuta ya visukuku.
- Toza ushuru ili kuzuia uzalishaji au matumizi ya plastiki inayotumika mara moja, au kutoa mapumziko ya ushuru, ruzuku na vivutio vingine vya kifedha ili kuhimiza njia mbadala. Kwa mfano Uingereza imeanza kutoza ushuru utengenezaji wa plastiki mpya. Mapato kutoka kwa ushuru huu yanaweza kutumika kuongeza ukusanyaji, kupanga na ujenzi wa miundombinu ya uchakataji wa plastiki.
- Wawajibishe watengenezaji wa mitindo mipya na wauzaji rejareja kwa takataka wanazozalisha. Mfano mmoja ni Sheria ya Mitindo, mswada mpya uliowasilishwa na wabunge wa Jimbo la New York. Unashughulikia madhara ya kijamii na kimazingira yanayotokana na tasnia ya mitindo.
- Kujiunga na Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu Uchafuzi wa Plastiki na Takataka za Baharini, na utumie jukwaa la kidijitali kuungana na wanaharakati wengine, kubadilishana maelezo na kuonyesha juhudi zilizofanywa na mafunzo yaliyopatikana.
- Kuimarisha ushirikiano wa tasnia mbalimbali ili kuanzisha na kudhibiti viwango rasmi vya kuwasilisha data kuhusu uchumi wa unatumia bidhaa tena na tena. Mpango wa Kusawazisha Data ya Utumiaji wa Bidhaa tena na tena ni mfano mmoja mzuri.
- Wekeza katika uboreshaji wa mitambo ya kusafisha maji chafu, ili mikroplastiki ziweze kuondolewa kutoka kwa uchafu.
- Tumia sera kuondoa upakiaji usiohitajika, kuzuia upakiaji kupita kiasi na uwekaji wa lebo wazi ili kusaidia uchakataji mwafak. Umoja wa Ulaya unalenga kufanya vitu vyote vinavyotumika katika upakiaji wa chakula viweze kuchakatwa kufikia mwaka wa 2030.
- Kupitisha sheria bunifu. Kwa mfano, katika mwaka wa 2020, Ufaransa ilikuwa nchi ya kwanza kuanzisha sera inayohitaji mashine zote mpya za kuosha zinazotumiwa nyumbani ziwe na vichungi vya kunasa chembe ndogo za plastiki kufikia mwaka wa 2025.
- Ili kuwa na athari kubwa zaidi, tumia mbinu mbalimbali zilizotajwa hapo juu na uzibadilishe kulingana na nchi yako. Hakuna mtindo mmoja mkubwa maalum wa kukabiliana na uchafuzi wa plastiki, ingawa ni muhimu kutekeleza mbinu jumuishi inayojumuisha mzunguko mzima wa maisha.
- Kushiriki katika shughuli za ziada, kama vile kuanzisha ushirikiano wa sekta ya umma na ya kibinafsi, kuzindua mipango ya elimu kwa wateja na kusasisha mahitaji ya ununuzi wa umma.

# Majiji, miji na serikali za mitaa

**Majiji, miji na mamlaka za mitaa zinaweza kuwa mstari wa mbele kuleta mabadiliko kwa kubuni sheria za mitaa, kusaidia biashara na kuhimiza tabia endelevu ya watumiaji bidhaa kupitia kampeni za uhamasishaji.**

- Kujenga mifumo thabiti zaidi, yenye ufanisi ya uchakataji na kushughulikia takataka. Udhibiti duni wa takataka mango ya manispaa ni mojawapo ya njia kuu zinazochangia uchafuzi wa plastiki kwenye ardhi na maji.
- Kujiunga na Mpango wa Kupunguza Uchafuzi wa Plastiki Katika Majiji, ambao huhamasisha majiji na maeneo kuzuia utupaji wa plastiki kwenye mazingira asilia.
- Kukuza na kutuza utengenezaji wa bidhaa utakaokosha bidhaa na mifuko ya plastiki inayotumika mara moja na kuhimiza matumizi ya uchumi unaotumia bidhaa tena na tena kati ya watoa huduma mijini.
- Kupitisha sheria ya kupiga marufuku matumizi ya bidhaa za plastiki zinazotumika mara moja, kama vile mifuko ya plastiki, mirija na vikombe, na kuhimiza matumizi ya bidhaa mbadala zinazoweza kutumika tena.
- Kupiga marufuku uchomaji taka katika maeneo wazi na kuimarisha hatua za utekelezaji.
- Kuweka maeneo ya umma ya kupata maji bila malipo ili kuhimiza watu waepuke kutumia chupa za plastiki za maji zinazotumika mara moja.
- Kuhimiza uwajibikaji pana wa wazalishaji katika ngazi ya mitaa ili wauzaji rejareja na wazalishaji wanaouza bidhaa za plastiki wawajibikie uchafuzi unaosababishwa na bidhaa zao.
- Kuunga mkono kampeni za tabia na mabadiliko ya kijamii za jiji zima ili kudhibiti vyema plastiki.


UNEP

# Fedha



Dreamstime

**Wawekezaji wanaweza kutekeleza wajibu muhimu katika kutafuta fedha na kuweka viwango kwa biashara na viwanda kuhamia kwenye uchumi unaotumia bidhaa za plastiki tana na tena.**

- Jisajili kwenye Kanuni za Umoja wa Mataifa za Uwajibikaji wa Benki na Kanuni za Bima Endelevu ili kuharakisha mabadiliko chanya ya kimataifa kwa watu na mazingira.
- Kuweka malengo ya kufadhili miradi inayotumia rasilimali vyema na tena, shughuli na wateja kwa kutumia Ahadi Mpya ya Uchumi wa Plastiki Ulimwenguni.
- Jiunge na Kikundi cha Uongozi wa Fedha kuhusu Plastiki ili kufuatilia maendeleo ya zana ya INC na kuitekeleza katika sekta zote za fedha duniani.
- Kushirikiana kwa njia nzuri na makampuni yanayoshughulikia mifuko ya upakiaji ya plastiki ili kubaini jinsi wanavyodhibiti hatari na fursa zilizoko zinazohusiana na upakiaji wa plastiki. Wahimize:
  - kukomesha uzalishaji na matumizi ya plastiki iletayo matatizo au isiy-ohitajika;
  - kuvumbua ili kuhakikisha kuwa plastiki zote zinaweza kutumika tena, kuchakatwa, au zinazoweza kuoza; na
  - kusambaza vifaa vya kuweka plastiki ndani ya uchumi na nje ya mazingira.

# Biashara na viwanda

**Ikizingatiwa kuwa kampuni 20 zinazalisha zaidi ya nusu ya plastiki zinazotumika mara moja duniani, mabadiliko muhimu yanahitajika katika jinsi biashara na viwanda vinavyozalisha, kutumia na kutupa plastiki. Kuna mambo kadhaa ambayo biashara na viwanda vinaweza kufanya ili kupunguza uzalishaji na matumizi ya plastiki.**

- Kubuni jinsi ya kushughulikia taka kwa kondoa na kutoa njia mbadala kwa uzalishaji na mifuko hatari ya plastiki isiyohitajika, hasa plastiki zinazotumika mara moja.
- Kupunguza kiasi cha takataka za plastiki zinazozalishwa wakati wote wa shughuli, hasa katika uzalishaji na upakiaji.
- Kuboresha muundo na uzalishaji wa plastiki ili kuhakikisha kuwa bidhaa zinaweza kutumika tena, zinazotumia rasilimali kidogo na zinaweza kuchakatwa kwa ufanisi.
- Kupunguza gharama kupitia utumiaji mzuri zaidi wa plastiki, kutafuta vyanzo vipya vya mapato kupitia miundo ya biashara ya 'mzunguko bora' ambayo hurejesha plastiki kama nyenzo muhimu na kupata wateja wapya kwa kuonyesha bidhaa endelevu zaidi.


Unsplash

- Kutumia teknolojia zinazoibuka ili kubuni masuluhisho yenye faida kwa uchafuzi wa plastiki yanayounga mkono malengo ya kimazingira, kijamii na utawala.
- Kufichua maelezo zaidi kuhusu kiasi cha plastiki kinachotumika katika bidhaa, ikiwa ni pamoja na plastiki zinazozalishwa kila mwaka, pamoja na kemikali zinazotumika katika plastiki.
- Kuhakikisha kuwa nguo za plastiki kama vile poliesta zinazotumiwa kutengenezea nguo zinachakatwa na wala sio kutupwa.
- Kubadili kutoka kwa plastiki hadi kwenye matumizi ya matandazo katika kilimo na kukumbatia masuluhisho yanayotegemea mazingira, kama vile mimea ya kufunika udongo, ambayo hulinda udongo dhidi ya mmomonyoko wa udongo, magugu na wadudu.
- Jiunge na mamia ya mashirika mengine ya biashara duniani kote katika kujitolea kuchukua hatua za kushughulikia mzunguko mzima wa plastiki kupitia Ahadi Mpya ya Uchumi wa Kimataifa wa Plastiki ili kuondoa, kuvumbua na kusambaza plastiki.
- Jiunge na Mpango wa Kimataifa wa Kupunguza Matumizi ya Plastiki katika Utalii, unaolenga kuondoa matumizi yasiyohitajika ya plastiki na kuhamia kwenye bidhaa zinazoweza kutumika tena.

# Je, uchafuzi wa plastiki unaathiri vipi bayoanuwai, tatizo la tabianchi, wanyamapori, na afya ya binadamu?

## Bayoanuwai

Takriban tani kati ya milioni 19 na milioni 23 za plastiki huingia katika mifumo ya ekolojia ya majini kila mwaka. Uchafuzi wa plastiki una madhara makubwa kwa viumbe vingi katika bahari zetu, mito, na nchi kavu. Takataka za baharini hudhuru zaidi ya spishi 800. Zaidi ya asilimia 90 ya ndege na samaki wote wanaaminika kuwa na chembe za plastiki kwenye matumbo yao. Madhara ya kumeza mikroplastiki ni makubwa sana; husababisha njaa, kuvurugika kwa mfumo wa endokraini, kudumaa kwa ukuaji katika baadhi ya spishi na uharibifu wa mifumo ya usagaji chakula. Plastiki inaweza kuzuia viumbe vya majini kupata oksijeni na mwangaza, vilevile mikroplastiki pia zinaweza kujaa kwenye udongo kutokana na matumizi yao katika bidhaa za kilimo.

## Tatizo la tabianchi

Uzalishaji wa plastiki ni mojawapo wa mchakato wa utengenezaji unaotumia nishati nyingi zaidi duniani, jambo ambalo ni changamoto tunapohitaji kufikia lengo la Mkataba wa Paris la kupunguza ongezeko la joto ulimwenguni lisizidi nyusijoto 1.5°. Katika mwaka wa 2019, plastiki ilizalisha tani bilioni 1.8 za GHG – asilimia 3.4 ya jumla ya kimataifa – huku asilimia 90 ya uzalishaji huo ukitoka kwa uzalishaji wa plastiki na ubadilishaji wa mafuta ya visukuku. Plastiki nyingi zinatokana na mafuta ya visukuku na tasnia ya plastiki huchangia asilimia 6 ya matumizi ya mafuta duniani. Kiwango cha uzalishaji wa GHG kinachohusiana na uzalishaji, matumizi na utupaji wa plastiki za kawaida zinayotokana na mafuta ya visukuku kinatabiriwa kukua hadi asilimia 19 ya uzalishaji wa gesi ya ukaa duniani kufikia mwaka wa 2040. Hili ni tatizo haswa la plastiki zinayotumika matumizi moja: Asilimia 98 ya bidhaa za plastiki zinazotumiwa mara moja huzalishwa kutoka kwa mafuta ya visukuku au malighafi.

## Afya ya binadamu

Mikroplastiki zinaweza kuingia ndani ya mwili kwa kuvuta pumzi na kuingia kupitia kwenye ngozi na kujilimbikiza kwenye viungo, ikiwa na pamoja na plasenta. Baadhi ya kemikali zilizo katika mikroplastiki zinahusishwa na madhara makubwa ya afya, hasa katika wanawake. Wanasayansi wamepata uhusiano kati ya kukumbana na vitu vinavyoongezwa kwa kemikali ambavyo hutoka kwenye plastiki na unene kupita kiasi, kisukari, afya mbaya ya ubongo na hata saratani. Utafiti bado unafanywa kuhusu athari za mikroplastiki kwa afya ya binadamu, na bado hatujui ukubwa wa jinsi zilivyo hatari. Zaidi ya hayo, kutokana na miundombinu ndogo na isiyotosha ya ushughulikiaji wa takataka, asilimia 40 ya takataka duniani huchomwa, asilimia 12 ya takataka hizi huwa ni plastiki. Uchomaji wa taka za plastiki una athari nyingi za kiafya, ikiwa ni pamoja na kuongeza hatari ya kupata magonjwa ya moyo na kuzidisha matatizo ya kupumua, kama vile pumu na ugonjwa wa kuvimba mapafu.

## Mikroplastiki ni nini?

**Microplastiki ni vipande vidogo vya plastiki ambavyo hutoka kwa vyanzo mbalimbali, vikiwemo magurudumu, nyasi bandia, vitambaa, bidhaa za afya na urembo (ambazo zina shanga ndogo), uvujaji kutoka kwa michakato ya utengenezaji wa viwanda na kilimo, na zana za uvuvi zilizoachwa, zilizopotea au kutupwa.**


# Je, takataka hizi zote za plastiki hutoka wapi?



Takriban asilimia **36** ya plastiki zote zinazozalishwa ni za kufungia bidhaa.

Takriban tani **bilioni 100** za taka kutoka kwa sekta ya majengo na ujenzi huzalishwa kila mwaka na takriban asilimia **35** huingia ardhini.







Zaidi ya kilo **milioni 45** za plastiki huingia baharini kutoka kwa zana za uvuvi wa biashara tu.



Magari hutengenezwa na takribani asilimia **30** ya vifaa vya plastiki.



Plastiki inayotumika katika sekta ya watumizi wa bidhaa inakadiriwa kuwa dola za Marekani **bilioni 75** kugharamia uharibifu wa mazingira kwa mwaka.



Plastiki inayotumika mara moja hutengenezwa zaidi kutoka kwa fueli ya visukuku, na uzalishaji wa plastiki unachangia takriban asilimia **3.4** ya uzalishaji wa gesi ya ukaa duniani.



Watalii wanane kati ya 10 hutembelea maeneo ya pwani, na kuchangia kwa tani **milioni 8** za plastiki zinazoingia baharini kila mwaka.



Takriban asilimia **60** ya nyenzo za kutengenezea nguo ni za plastiki. Ufuaji pekee husababisha takriban tani 500,000 kujikuta baharini kila mwaka.



Takriban tani **milioni 12.5** za bidhaa za plastiki hutumika katika ukuzaji wa mimea na wanyama, na tani **milioni 37.3** katika kufungia vyakula kila mwaka.

## Upakiaji

Sekta ya upakiaji ndiyo [chanzo kikuu zaidi duniani cha takataka za plastiki zinazotumika mara moja.] Takriban asilimia 36 ya plastiki zote zinazozalishwa ni za upakiaji. Hii ni pamoja na mikebe au chupa za chakula na vinywaji zinazotumiwa mara moja, asilimia 85 yake huishia kwenye dampo au kama takataka hatari.

## Utengenezaji wa Bidhaa

Plastiki hupatikana katika kila kitu kutoka kwa magari na vifaa vya elektroniki hadi vifaa vya matibabu na vitu vya watoto kuchezea. Bidhaa hizi hujumuisha viungo vya kemikali ambavyo vinaweza kutoka na kuathiri afya ya wanyama na mimea. Plastiki inayotumika katika tasnia ya bidhaa za matumizi husababisha uharibifu wa mazingira wa takriban dola bilioni 75 za Marekani kwa mwaka.

## Majengo na ujenzi

Nyenzo za kawaida za ujenzi, kama vile mabomba, sakafu, na rangi zina plastiki. Hizi huwa takriban asilimia 35 ya jumla ya matumizi ya plastiki. Takriban tani bilioni 100 ya takataka kutoka kwa viwanda huzalishwa kila mwaka na takriban asilimia 35 hutupwa kwa dampo la takataka.

## Kilimo

Plastiki hutumiwa sana katika mifumo ya ukulima na kilimo. Takriban tani milioni 12.5 za bidhaa za plastiki hutumiwa katika ukuzaji wa mimea na wanyama, na tani milioni 37.3 katika upakiaji wa chakula kwa mwaka.

## Uvuvi

Inakadiriwa kuwa asilimia 20 ya plastiki yote baharini hutoka kwa uvuvi, usafirishaji wa meli na shughuli za burudani. Zaidi ya kilo milioni 45 za plastiki huingia baharini kutoka kwa zana za uvuvi wa biashara tu. Vitu hivi, kama vile neti, vinaweza kunasa na kuua viumbe vya baharini na kuchafua bahari kwa kuweka mikroplastiki.

## Nishati, mafuta na gesi

Kampuni ya nishati ni baadhi ya wachafuzi wakuu wa plastiki duniani. Plastiki inayotumika mara moja inatengenezwa kutoka kwa mafuta ya visukuku, na uzalishaji wa plastiki huchangia takriban asilimia 3.4 ya uzalishaji wa gesi ya ukaa duniani. Kiwango hiki kinakadiriwa kuongezeka wakati kampuni ya kemikali ya mafuta zinapobadilisha bidhaa zao kutoka kwa nishati hadi plastiki.

## Nguo na mtindo


Ulimwengu unazalisha na kutumia nguo nyingi zaidi kuliko hapo awali. Takriban asilimia 60 ya nyenzo zinazotumiwa kutengeneza nguo ni za plastiki. Nguo zinapooshwa, vipande vinatoa nyuzi ndogo ndogo – aina ya mikroplastiki. Ufuaji pekee husababisha takriban tani 500,000 kumwagwa baharini kila mwaka, ambayo ni sawa na karibu mashati bilioni 3 ya poliesta.

## Usafiri na utalii

Utalii huchangia pakubwa katika tatizo la kimataifa la uchafuzi wa plastiki. Watalii nane kati ya 10 hutembelea maeneo ya pwani, na kuchangia kwa tani milioni 8 za plastiki zinazoingia baharini kila mwaka. Hoteli nyingi pia zimejaa shampuu, miswaki na vichana vya plastiki vinayotumika mara moja. Huku meli za kitalii zikimwagaga kiasi kikubwa cha maji chafu yaliyojaa mikroplastiki baharini.

## Uchukuzi

Magari yanatengenezwa kwa karibu asilimia 30 ya vitu vya plastiki. Lakini nyingi ya plastiki hii huenda kwenye dampo kwani imetengenezwa kutoka kwa polima za bei nafuu. Badala yake, sehemu za chuma zenye thamani au vitu vya kielektroniki huondolewa.



# Hatua gani zimepigwa?

## Maelezo ya ziada: Je, uchakataji ni suluhu?

Takataka nyingi zaidi za plastiki hazishughulikiwi ipasavyo badala ya kuchakatwa na makadirio ya kimataifa ya uchakataji bado yako chini. Ulimwenguni kote, asilimia 46 ya takataka za plastiki hutupwa kwenye dampo, asilimia 22 huwa takataka, asilimia 17 huchomwa na asilimia 15 hukusanywa ili kuchakatwa, na chini ya asilimia 9 huchakatwa baada ya kupotea kwa kiasi fulani.

Utumiaji wa plastiki tena na tena unahitaji kuongeza kasi kwa wakati mmoja kwa mabadiliko matatu ya soko: kuzitumia tena, kuchakata na na matumizi mapya na matumizi mbalimbali ya kubadilisha plastiki kwa njia mbadala zilizo endelevu zaidi. Kwa hivyo, ingawa uchakataji ni sehemu moja ya suluhisho, kunahitajika kuwe na mabadiliko ya kimfumo ili kuwa na uchumi unaotumia bidhaa tena na tena .




Hatua fulani zimepigwa katika kukabiliana na uchafuzi wa plastiki, lakini ahadi za sasa za serikali na viwanda zitapunguza kiwango cha mwaka cha plastiki inayotiririka baharini kwa takriban asilimia 8 tu kufikia mwaka wa 2040. Kanuni nyingi mpya huzingatia vitu maalum badala ya mabadiliko ya kimfumo na hazizuii kwa kiasi kikubwa makadirio ya ukuaji wa uzalishaji wa plastiki. Jitihada za sasa zinalenga hasa kuchakata au njia za kutupa plastiki lakini juhudi kubwa zinahitajika pia ili kuondoa plastiki hatari na uvumbuzi na vivutio vinahitajika ili kuzibadilisha na chaguo zilizo nzuri kwa mazingira. Hatua hizi nyingi zitahitajika kufanywa na serikali. Na ingawa kumekuwa na ongezeko la sheria ya kupiga marufuku mifuko ya plastiki, kunahitajika kuwepo na mabadiliko ya kimfumo katika njia tunayozalisha, kutumia na kuweka plastiki katika uchumi.

Mipango kadhaa imeshika kasi katika miaka michache iliyopita, ikihusisha sekta ya plastiki, biashara tofauti, serikali, mashirika ya kimataifa na mashirika ya uraia kubuni masuluhisho ya kukomesha uchafuzi wa plastiki. Hii ni pamoja na Ahadi Mpya ya Kimataifa ya Uchumi wa Plastiki inayoongozwa na Wakfu wa Ellen MacArthur kwa ushirikiano na UNEP, ambayo inaunganisha zaidi ya mashirika ya biashara 500, serikali na mashirika mengine yanayolenga kujenga uchumi unaotumia bidhaa za plastiki tena na tena, pamoja na Ushirikiano wa Kimataifa wa Uchafuzi wa Plastiki na Uchafuzi wa Bahari ambao naunganisha zaidi ya wahusika 600.

Katika mwaka wa 2022, Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa zilikubaliana kuhusu azimio la kubuni makubaliano ya kisheria ambayo yatakomesha uchafuzi wa plastiki kufikia mwaka wa 2024. Kimsingi, hili linajumuisha hatua zinazozingatia mzunguko mzima wa plastiki, kutoka kwa uzalishaji hadi muundo wa bidhaa hadi ushughulikiaji wa takataka, kuwezesha fursa za kubuni njia za kuondoa takataka kabla hazijaundwa kama sehemu ya uchumi unaostawi. INC kwa sasa inaandaa makubaliano hayo.

## Maelezo ya ziada: Je, suluhu ni vitu vinavyoweza kuoza?

Ingawa plastiki nyingi zinazouzwa husemekana kuwa zinaweza kuoza, ukweli ni kuwa plastiki ni ngumu zaidi kuoza.

Kuoza kamili kwa plastiki hutokea wakati hakuna polima ya awali inayobakia, mchakato ambao vijidudu huvunja plastiki kuwa kaboni dioksidi, methani na molekuli za maji. Mchakato huo unategemea halijoto na baadhi ya plastiki zinazorejelewa kuwa 'zinazoweza kuoza' zinahitaji hali ambazo kwa kawaida hutokea katika vitengo vya kuozesha viwandani, zenye halijoto ya muda mrefu ya zaidi ya nyuzijoto 50, ili kuvunjwa kabisa. Hali kama hizi ni nadra sana ikiwa zimewahi kufikiwa katika mazingira. Ubaya zaidi wa kuenea zaidi kwa matumizi ya plastiki 'zinazoweza kuoza' ni haja ya kuzitenganisha na mikondo ya takataka zisizoweza kuoza kwa ajili ya kuchakata plastiki ili kuepuka kuharibu ubora wa bidhaa ya mwisho. Aidha, kuna baadhi ya ushahidi wa kupendekeza kuwa kurejelea bidhaa kama 'inayoweza kuoza' kutasababisha mwelekeo mkubwa wa kutupwa kwa upande wa umma.

# Ni nini kingine kinachohitajika kufanywa?

Hatua zaidi zinahitajika, ikiwa ni pamoja na kupunguza uzalishaji na matumizi ya plastiki; kubadilisha sekta nzima; utungaji wa sheria bora, uwazi, na zinazoweza kuleta mabadiliko kwa haraka, na mifumo ya ufuatiliaji yenye ufanisi zaidi ili kubainisha vyanzo vya plastiki, kupunguza huku tukihamia njia za kutumia tena. Hakuna suluhisho moja la kipekee, lakini nyingi lazima zitumike kwa wakati mmoja na mara moja.

**Shinikizo la watumiaji ni muhimu, lakini hatua halisi zinahitajika kutoka kwa kampuni, wawekezaji, watunga sheria na serikali.**

Kuhamia njia za kutumia tena na tena na njia mbadala za matumizi yaplastiki ni muhimu. Hii inahusisha mbinu ya kuzingatia mzunguko mzima – moja ambapo athari ya shughuli zote na matokeo yanayohusiana na uzalishaji na matumizi ya plastiki huzingatiwa. Hii ni pamoja na kutathmini upya uchimbaji na usindikaji wa malighafi, na kuvumbua michakato ya utengenezaji, upakiaji, usambazaji na usimamizi wa mwisho wa matumizi, kama vile kutenganisha, kukusanya, kupanga, kuchakata na utupaji.

**Kukabiliana na uchafuzi wa plastiki kunahitaji mabadiliko ya kimfumo, na hatua katika mzunguko mzima kwa kushughulikia vyanzo vyake badala ya athari zake.**

**Hii ni changamoto kubwa, lakini moja tunayopaswa kuitatua.**



UNEP / Duncan Moore, Florian Fussstetter

*Mwongozo huu wa Vitendo wa Hatua za Kukabiliana na Uchafuzi wa Plastiki uliten-genezwa kama sehemu ya Siku ya Mazingira Duniani mwaka wa 2023, kwa kuzingatia masuluhisho kwa uchafuzi wa plastiki.*

**Kwa taarifa zaidi**
worldenvironmentday.global/sw
worldenvironmentday@un.org
unep.org/sw
United Nations Avenue, Gigiri, PO Box 30552, 00100 Nairobi, Kenya

KOMESHA UCHAFUZI WA PLASTIKI | SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI | UN environment programme | Republic of Côte d'Ivoire | Supported by Ministry of Infrastructure and Water Management of the Netherlands